# MUHTASARI WA SEMINA YA TAASISI YA BIBLIA NA UTUMISHI MOROGORO
# TAREHE 18/11/2014

**MATUKIO YA ASUBUHI**

Toka CCT sanga sanga.

1. Kufika.
2. Chai – mkate uliopakwa blueband - sio wanasemina wote wanaotumia blueband - hivyo basi mikate isipakwe yote.
3. Darasani.
4. Mwenyekiti - Rev. Falanta.

- Wimbo - Mrs Sanagu.
- Neno:-3:14-17

  Mwj. Esther Mika alitoa ujumbe kwa kifupi. Fundisho kuu lilikuwa '***tusiwe vuguvugu'*** tusije tukatapikwa/kuachwa na Mungu. Tuwe na msimamamo katika Bwana na utumishi pia.

  Maombezi - Ujenji wa nyumba ya mtumishi Babati, Manyoni:- ununuzi wa viwanja mgandu (wagonjwa Maria kuhanda) shukrani:- Wanasemina kufika salama.

Baada ya maombi mwenyekiti wa Taasisi aliwaomba wanasemina kuchagua uongozi wa semina. Walikubali ombi hilo na kuwachagua wafuatao:-

- **MWENYEKITI:-** MCH. MUSSA LUZALI
- **KATIBU:-** MWJ. H. NDARO
- **AFYA:-** MCH. ISEBUKA NA MAMA KAMOYO.
- **TIMEKEPEER:-** MCH. SHILIKALE.

Baada ya uchaguzi huo Mchungaji Sanagu alitoa taarifa ya kufariki kwa Dr. Magadula (mzee wa kanisa la AICT Changanyikeni). Baada ya taarifa hiyo ya kusikitisha, mwenyekiti alimwomba mch. Ndaro kuomba kwa ajili yafaraja kwa familia hiyo na kanisa kwa ujumla. Kisha mama Joyce Mfeti aliomba kwa ajili ya chai.

**<u>KUFUNGUA SEMINA</u>**

Baba Askofu Charles Salalah aliwaasa watumishi kuwa, Matarajio yake ni kwamba masomo yote tunayojifunza katika Taasisi hii:-

- Yasiwe mazoea tu bali yalete mabadiliko katika maisha ya mtu binafsi na utumishi pia. ***'Elimu yoyote isiyolete mabadiliko haina faida.'*** Hivyo basi, ukijua, ni heri ukitenda.
- Wale wenye makanisa makubwa wasiwe na tabia ya ***Tembo*** (yaani kujikusanyia wenyewe tu *ubinafsi*, badala yake mafundisho haya yawasaidie kufumbua macho na kuwashirikisha wengine vipawa na baraka mbalimbali walizo nazo). Kisha alifungua semina rasmi kwa Jina la **Mungu Baba, mwana na Roho Mtakatifu.**

**Baada ya ufunguzi yalifuata mapumziko ya muda mfupi na chai kavu.**

- Mchungaji Bethuel Hanje aliomba kwa ajili ya kumkaribisha mwalimu , Mch. Dr. Tony Sargent
- Lakini kabla ya kuanza kipindi, Mch. Falata alimtambulisha Dr. Wilson Mtebe kisha aliomba radhi kwa kusahau kumtambulisha mama askofu wakati wa kumtambulisha baba askofu . Ndipo alitumia nafasi hii kumtambulisha na kusema matarajio yake katika semina hiyo.

- Dr.Tony Sargent aliomba pambio la kuchangamsha wanasemina.
- Dr. T. Sargent alianza kwa salamu, kisha akawakumbusha wanasema machache juu ya semina ya mwaka 2012.
- Alimshukuru Mungu jinsi Mungu alivyomtumia sehemu mbalimbali na akatamka wazi atalipia gharama zote za umeme katika eneo la Taasisi ya Biblia na Utumishi hapa Sangasanga. Wanasemina walifurahi na kumpongeza kwa makofi na vigelegele.
- Kisha Dr. Sargent aliendelea kwa kutumia mfano wa msamaria mwema.

NB: Somo kuu pale ni kwamba kile ambacho ametupatia ni chake Mungu na anahitaji tutumie na wengine.

Mungu alikuwa na kusudi na mji wa Ninawi ndio maana alimtuma Yona.

- Mungu alikuwa na kusudi na mji wa Yerusalemu, ndiyo maana alimtuma Nehemia.
- Wakati Kipindi kikiendelea, Rev. Swanson alichora picha ya simu ubaoni na kuweka alama ya X ili kuwakumbusha wanasemina kuzima simu zao.

**FUNDISHO**

- Nehemia aliona jinsi mji ule ulivyo kuwa na hakukaza macho yake kuona vile ilivyokuwa tu bali alikaza macho yake kuona jinsi itakavyo kuwa ."See things, what they are and what they should be." NB: Focus on what they should be, this is what Nehemiah did.
- **Key verse is Nehemiah 1 :3**
- Nehemia alipoona uzito wa kazi ile na mzigo aliokuwa nao, ulimsukuma kulia.
- Kama unataka kuwa na huduma yenye nguvu mahali popote unapotumika mlilie Mungu kama Nehemiah. ( mst 4 )
- Siyo kulia tu bali pia kufunga, kuomboleza na kuomba.(mst 4 )
- Maombi ya kufunga ni maombi yenye nguvu na mafanikio makubwa.
- Nehemiah ni mfano mzuri sana wa kuigwa kwa maombi ya kufunga.
- Tusipumzike kumwomba Mungu mpaka tutakapojibiwa.
- Tuombe kwa ajili ya Tanzania, kanisa nk.
- Tunaposimama mbele za Mungu kwa maombi, tunapata nguvu ya kusimama mbele za watu na kuaminiwa.
- Kumbuka kuwa watoto 1million wanasafirishwa kila mwaka (human traffic), Je, tunajua hivyo, na tunafanya nini kama kanisa? Kanisa la Kristo leo lina nguvu katika Afrika tukiwa na umoja, kuujua wajibu wetu na kusimama imara kama Nehemiah bila woga tutaleta mabadiliko makabwa kanisani, taifa na ulimwengu kwa ujumla.

**KAZI YA VIKUNDI**

Baada ya kipindi cha kwanza, wanasemina waligawanyika katika vikundi na kujadili yaliyomo katika kitabu cha Nehemiah.

- JUMLA YA VIKUNDI- 10.

Nehemiah alikuwa na mzigo, Je, tuna mizigo kwa ajili ya kazi maalumu ambayo Mungu ameweka mioyoni mwetu?

- Kila mwanasemina alijaribu kujilinganisha na Nehemia katika maono na utumishi wake.

**BAADA YA KAZI YA VIKUNDI:**

Kipindi kilifunguliwa kwa pambio la kusifu na maombi. Matangazo yafuatayo yalitolewa:- Idara ya afya ilisisitiza juu ya usafi na kutunza mazingira, pia ilionyesha chombo cha kuwekea uchafu. Mratibu (Tony)

Aliwakumbusha wanasemina juu ya kipindi cha michezo na umuhimu wake na kuwatia moyo kutumia fursa hiyo vizuri. Baada ya matangazo hayo mchungaji Isack Matinya aliomba kwa ajili ya chakula cha mchana. Baada ya chakula cha mchana, watu wote walipata mapumziko ya masaa mawili, jua lilikuwa kali sana, kivuli kilipatikana kwa shida na wengi wao walilala kwenye viti vyao.

Baada ya mapumziko, mwenyekiti aliwakaribisha wageni na kuwatambulisha. Miongoni mwao alikuwemo Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Pwani mzee Lucas Singili. Baada ya utambulisho huo mwanaseminai mmoja alituongoza wimbo wa kuabudu uliofuatiwa na maombi. Kisha Dr. Tony Sargent aliendelea na kipindi.

Somo lilitoka katika Nehemia sura ya pili. Mada kuu ilikuwa “Mungu ni wa pekee na anaweza kuchagua yeyote na kumtumia kwa kazi yake.” (Ezek.22:30). Dr. Sargent alitoa mfano wa Ask. Akudur wa Congo ambaye alipigwa na kupata majeraha ya ajabu wakati wa vita ya waasi, lakini alisimama imara na ushuhuda wa Kristo. Na kwa ajili ya uvumilivu na utii wake kwa Mungu, sasa kuna wakristo wengi na anakumbukwa sana.

Kabla ya kuujenga ukuta , lazima tusimame katika pengo. Ukuta tunaopaswa kuujenga leo ni wa Kiroho (kanisa). Tunapaswa kuelewa kuwa, tunapoanza kuyafanya mapenzi na kazi ya Mungu iliyo na Baraka daima kuna upinzani kama ilivyokuwa kwa Nehemia, Yusufu na Yesu mwenyewe. Tusikate tamaa bali tuwe na mkakati na kuusimamia. Mfumo wa utenda kazi ni ule ule tu. Tunapaswa kuwa na **Maono, mzigo,mikakati, ratiba,kushirikisha wengine, kujiamini na kuwajibika kikamilifu**. Mwisho, Dr. aliwaomba wasemina kuiombea nchi ya Tanzania, na yeye alifunga kipindi kwa maombi.

Baada ya mafundisho hayo, mchungaji Tony alitoa matangazo kama kawaida, kisha Kiongozi wa michezo (Mchg. Makunza), alisema kuwa leo hatutakuwa na michezo bado vifaa havijaandaliwa. Hivyo basi, muda wa michezo tutautumia kuzunguka na kuangalia eneo la Taasisi ya Biblia na Utumishi. Baada ya kipindi hicho, kilifuatia kipindi cha maombi ya jioni kikifuatiwa na chakula cha usiku. Kisha safari ilianza ya kurudi kambini (CCT). Huo ulikuwa ni mwisho wa siku ya kwanza.

**SIKU YA PILI TAR. 19/11/2014**

Mwenyekiti alifungua kipindi kwa nyimbo mbili, kisha wanasemina walitaja mambo ya kuombea kama ifuatavyo:-

1. Mama Mwj. Makeja (aliyegunduliwa kuwa na kansa ya utumbo)
2. Mauaji Wilaya ya Kiteto kati wa wafugaji na wakulima (watu 7 tayari wameuwawa)
3. Taifa na chaguzi za serkali za mitaa hadi ngazi ya Taifa
4. Afya ya Rais Jakaya Kikwete
5. Shukrani kwa ajili ya afya zetu
6.

**Waombaji:-** Mama Askofu Salalah, Mama Mchungaji Nyamalya na Mchungaji William Mfeti.

Baada ya maombezi, mwenyekiti aliwakaribisha wageni, kisha Dr.Tony Sargent aliendelea na mafundisho.

- SOMO:- NEH. 3 & 4
- **Fundisho kuu:-**Nehemia amewaunganisha watu wengi katika kuifanya kazi yake maana Yerusalem ilikuwa na malanngo mengi. Hivyo basi, AICT pia tunahitaji kuwa na ushirikiano na sisi kwa sisi na watu wengine pia katika kuifanya kazi ya Mungu. Pia katika kazi hii tusiwasahau wanawake maana ni wa muhimu sana, Mungu ameita wote wanaume na wanawake kama ilivyokuwa kwa Malkia Esther.
- Baada ya kipindi hiki, tulienda pumziko. Na baada ya pumziko Dr. Sargent aliendelea na kufafanua malango **10** yaliyotajwa katika sura ya tatu na kila lango na maana na fundisho lake (**lango kondoo**- Yesu ndiye mlango wa kondoo, **lango la samaki**- tumeitwa kuwa wavuvi wa

watu, **lango la kale**- halikufanyiwa matengenezo- ni neno la Mungu ambalo halihitaji matengenezo, **lango la bondeni-**mahali pa mateso na matatizo katika kumfuata yesu, **lango la chemchemi**- Yesu ndiye chemchemi ya maji uzima, **lango la jaa**- Yesu aliye mahali maovu na dhambi hutupelekwa, **lango la maji,** neno la Mungu husafisha, **lango la farasi**- ushindi, **lango la mashariki** na **lango la gereza**- mahali pa hukumu ya milele).

- Malango haya yote ni utangulizi wa kuingia Yerusalemu, lakina pia yanatufundisha juu ya tabia zetu kiroho na namna ya kutengeneza mienendo yetu.
- Tunapofanya kazi ya Mungu tujue tunao upinzani kama Nehemia lakini tusikate tamaa.

Baada ya somo hili Dr. Sargent aliongoza maombi kwa ajili ya:-

- Iraq—Waislam wamjue Yesu
- Nchi ya Tanzania

**KIPINDI CHA PILI**
Mwezeshaji:- ASKOFU. CHARLES SALALAH
SOMO:- KUJITAMBUA MWENYEWE (self- awareness)
**SWALI LA KUFIKIRISHA:-** Je, vile unavyofahamika kwa mkeo, watoto, jamii, Kanisa na watu mbalimbali unaohudumu pamoja nao, wakiambiwa kutoa taarifa juu yako, taarifa hiyo itafanana?

Swali hili la utangulizi lilizua mjadala mkubwa. Baada ya mjadala huo, jibu lilikuwa ni 'HAPANA' kila kundi litakuwa na jibu lake kulingana na vile wanavyokufahamu na huduma yako kwa kundi husika.

**Mkazo:- jambo la muhimu, ni wewe mwenyewe kujitambua kuwa ni nani? Na utakapojitambua mwenendo na tabia yako ndiyo yawe maisha yako.**

**<u>KIPINDI CHA TATU</u>**

**SOMO:-** MKRISTO NA KAZI

**Mwezeshaji:-** MZEE JOHN KENNARD
MAANDIKO: Math.25:14-30; I Pet. 4:10

MAMBO SABA YA KUJIFUNZA

1. Mali tuliyo nayo siyo yetu, ni ya Bwana (mst.14, Hag.2:8,Zab. 24:1)
2. Tumepewa kwa kadiri ya uwezo wetu (mst.15). Talanta ni kitu cha thamani sana.Talanta moja ni sawa na mshahara wa miaka 100. Talanta moja ni sawa na million 200. Mungu anatugawia talanta kulingana na uwezo wetu (I cor. 3:5)
3. Tunapaswa kuwekeza tulichopewa na Mungu (Math.25:16). Ukiwekeza utapata zaidi na zaidi, usipowekeza utapata hasara hat ya kile ulichonacho (mst.18)
4. Siku ya kuwajibishwa inakuja (mst.19). Mungu atakagua kazi yetu na tutatoa habari za kazi zetu (Rum 14:12). Kristo anarudi tena, tufanye kazi kwa bidii kwa kadiri ya uwezo tuliopewa (I Yoh.2:28).
5. Tukitumia mali/talanta zetu vizuri tunapata furaha ya kutoa taarifa mbele za Mungu. (mst.20-23; Luk.6:38). Toa na utapokea kipimo kizuri.
6. Tusipotumia talanta/karama zetu vizuri tutalalamika na kusema uongo na kupata hasara (mst.25-26), 'Who you know and what you do, will bring you benefit or lose.' Ukilenga sifuli, utapata sifuli.
7. Nguvu imo katika kusonga mbele hata kama unajisikia una hofu na kuogopa. Jitie nguvu katika Bwana, nawe utapata nguvu ya kusonga mbele. (Mith.6:9; 10:5; 13:4; Hes.6:11-12).

**NB:** Watu wawili wa kwanza, walikuwa tayari kupokea talanta na kuchapa kazi hata kuhatarisha maisha yao, walipata faida.

Yule wa mwisho, hakumfahamu Bwana wake, hivyo hakujishughulisha kabisa. Alipata hasara kubwa. Sisi tunaomjua Mungu na ametuita kumtumikia, tukitii na kuyafanya mapenzi yake, tutapata faida. Lakini tusipomtumikia na kutumia vema talanta tulizopewa na Mungu tuna hasara kubwa sana. Mungu atusaidie.

**20/11/2014**

SOMO:- Neh. 6

**NENO KUU:--** Sisi sote ni wajenzi tuangalie jinsi tunavyojenga

Mwezeshaji:- Dr.Tony Sargent

Lutu aliokoka kutoka Sodoma lakini ni kama kwa moto. Hakupoteza uzima lakini kazi yake haikuacha matunda. Kanisa la leo linahitaji watendakazi walio na vifaa maalum vya kazi.

Mambo matatu waliyokuwa nayo Nehemia na wenzake:-

1. Walipewa akili ya kufanya kazi
2. Moyo wa kuomba
3. Macho ya kuona kazi ikiendelea lakini na upinzani pia (4:9). Tobia, Sanbalati na Geshemu walikuwa wapinzani wakubwa.

**Vifaa muhimu**

1. Upanga- Neno la Mungu
2. Koleo – Jinsi ya kutumia neno la Mungu kulingana na mazingira
3. Tarumbeta – kuliambia kanisa kwamba wawe macho maana kanisa linashambuliwa

MTUMISHI/MCHUNGAJI ANAPASWA KUJUA NA KUSIMAMA KIDETE NA KUWA MACHO NA YAFUATAYO:-

1. Mambo yanayokatisha tamaa
2. Kujua marafiki vigeugeu na kujiepusha nao
3. Kufundisha kweli ya neno la Mungu
4. Jiepushe na injili za utajiri/mafanikio
5. Usijitukuze mwenyewe, mtukuze Mungu
6. Mambo yanapokuzidi mwambie Mungu
7. Kubadilisha yale ambayo hayawezekani, yakawezekana (Neh.6:11). ‘Let oh No! became an oh Yes!’ Nehemia alikataa kubadilisha mapenzi ya Mungu.

**KIPINDI JIONI**

SOMO: KUJENGA KUPITIA MAHUBIRI (NEH.8:1-8)

Tuelewe kuwa tunaishi kwenye ulimwengu wenye falsafa tatu.

1. Chako ni changu na ninaweza kukichukua
2. Changu ni changu na nitakitunza
3. Kile ambacho nimeaminiwa na kukabidhiwa na Mungu nitashirikishana na ndugu wengine.

Kazi ya mhubiri ni kubwa maana inaleta ujumbe wa Mungu. Katika ibada mahubiri ni ya muhimu sana. Hivyo basi, lengo la mahubiri ni kugusa maisha ya watu na kuwaacha wamejisikia hatia, kusamehewa, kupokelewa na kukubaliwa na Mungu. (Neh.8:5).

Sisi wahubiri tunapaswa kujua kuwa tuna kazi kubwa:-

Tunapaswa kujiandaa vizuri kwa maombi na uongozi wa Roho Mtakatifu. Tazama ukuta wa Yerusalemu ulivyokuwa, Nehemia alivyoona na kufanya. Tuwe watu wa kuona na kufanya kazi ya Mungu ili kuleta mabadiliko bila kukata tamaa.

**IBADA NA MAOMBI YA USIKU**

Mwenyekiti alikaribisha kwaya ya wahitimu wa Nassa kwa wimbo mmoja, ambao uliinua hisia za watu. Baada ya wimbo huo mambo ya kuombea yalitajwa na wote kwa pamoja tuliyaombea.

1. Watakaosafiri kesho kurudi nyumbani kwao
2. Shukrani kwa ajili ya waliofanya mitihani ya kidato cha nne na safari zao za kurejea nyumbani
3. Shukrani kwa ajili ya Mchungaji Shikombe alipata ajali, magari yalikwaruzana, lakini wao hawakuumia.

Baada ya maombi tulipata chakula cha usiku kisha kurejea kambini.

**TAR. 21/11/2014**

Mwenyekiti alifungua kipindi kwa maombi kisha aliruhusu kwaya zifuatazo kumsifu Mungu;-

1. Imani kwaya (wahitimu wa Katungulu)
2. Tobotobo kwaya

Watu alifurahi sana, wengine walijiunga kuimba nao na wengine walitoa zawadi wakiongozwa **na Mama Tony.**

**MAOMBEZI**
- Jacob Matinya – alipokea ujumbe wa vitisho
- Peter Sabanya – alitekwa na majambazi huko Kibaha na kulazwa katika hospitali ya Tumbi Kibaha.
- Mama Kuhanda – Aling'olewa jino
- Wanafunzi wote—mitihani na afya zao
- Mchungaji Katwale—Hitaji la usafiri
- Wamisionari – hasa walio maeneo ya Uislam (kama Kwamadebe na Tanga)

**WAOMBAJI**
1. Mch. John Kamoyo
2. Mama Mch. John Sweya
3. Mchungaji Mesia Mbeyela

**KIPINDI CHA MWISHO CHA DR. SARGENT**

**MADA:-** Uislam ndiyo changamoto ya ulimwengu

Upinzani uliopo sasa ni kati ya:-
1. Yesu wa Nazareth
2. Mohamad toka Mecca
3. Biblia na Quran

NB: Ukristo na Uislam ni kama mito miwili inayokaribiana lakini kamwe haikutani (Fil.2)

Islam means ***Surrender***

***Obrogation***- Nguvu ya Uislam ni kwamba:- Ufunuo wa mwisho una nguvu kuliko kuliko ufunuo wa kwanza au uliotangulia. Waislam wanaamini kuwa Yesu wao yuko karibu kurudi na akirudi atawasaidia kuhubiri uislam. **Mungu anazungumza na waislam kwa njia ya ndoto na maono.**

**MAMBO YA KUJUA NA KUTUSAIDIA KUWAFIKIA WAISLAM**

i. Tufumbue macho yetu na kujua kile waislam wanachoamini na kuwafikia kwa Injili.
ii. Waislam wanateka kwa upanga, lakini wakristo wanateka kwa msalaba
iii. Tunapaswa kuwapenda na kujenga urafiki nao ili tuweze kuwashirikisha habari njema
iv. Watumishi tutafute na kusoma Quran (Lakini tunaposoma tusichore mistari kama tunavyofanya kwenye Biblia, maana muislam akiona hivyo utamkwaza. Yaani haujamweshimu Mungu.
v. Kuna kifungu kinatulinda katika Quran kinasema 'watu wa Injili lazima waheshimiwe.'

**MANENO YA KUAGANA**

**Dr. Tony Sargent** aliwaaga wanafunzi kwa maneno haya:-

Katika masomo yote tuliyojifunza, kila mara kiri kwamba "***Inawezekana"*** (ooh Yes, not oh No).

Kisha aliwashukuru wote kwa ushirikiano na kuahidi kuwa ataendelea kuomba na kushirikiana na Taasisi ya Biblia na Utumishi kwa hali na mali. Ikiwa ni pamoja na kulipa gharama za kuleta umeme kwenye eneo la Taasisi.

Askofu Charles Salalah, alimshukuru Mungu kwa ajili ya Dr. Sargent

**NASAHA ZA SHUKURANI ZA BABA ASKOFU.**

Alimshukuru Mungu kwa ajili ya Dr. Sargent na vile Mungu alivyomtumia safari hii katika kufundisha na kufafanua kitabu cha Nehemiah.

Mafundisho ya Dr. Sargent yanatusukuma kutenda sio kukusanya maarifa tu.

Pia alimshukuru kwa vile ameshiriki katika kuendeleza kituo hiki kama alivyoahidi. Alimalizia kwa kusema kuwa Mungu akipenda atakuwa pamoja nasi mwakani wakati tunaposherehekea miaka 20 ya AICT Dayosisi ya Pwani.

Mch. A Ndaro aliomba kwa ajili ya safari ya Dr.sargent (Uganda, Kenya).

**Maswali**

1. Watu wanaomwamini Yesu kutoka katika mazingira ya kiislamu wasaidiweje maana wengine hutengwa na jamii zao.
2. Waislamu wanaookoka na kutumwa kwenda kusoma na wanapomaliza wanaondoka, kanisa wafanyaje?

**KIPINDI CHA PILI ASKOFU SALALAH**

Muhtasari:-

1. Kuna ufa mkubwa kati ya vile tunavyofahamu/jitambua tunavyoishi/tenda tunavyoenenda.
2. Namna tunavyoweza kukabiliana/kuziba ufa huu Wafilipi. 3:7ff) tukaze mwendo.
    i. Neno la Mungu (hutupatia mwanga- illumination)
    ii. Roho Mtakatifu.
    iii. Tunategemeana/ hitajiana( mentorship).

NB: sisi watumishi  tunategemeana hivyo basi tusiwe watu wa vikundi vikundi bali tusaidiane kwa kuambiana ukweli.

Mifano ya watu wanaojitambua wenyewe katika Maandiko Matakatifu.

1. Daniel 1:8 (lazima uwe meneja wa maisha yako.)
2. Daniel na wenzake.
3. Daniel wakati wa mfalme Dario.
4. Yusufu katika nyumba ya Potifa.(Mwl. 39:1)
5. Mwana mpotevu.
6. Mhalifu pale mxsalabani.
7. Yuda Iskariote.(mat 27:3-5)

NB: tunapaswa kujitambua na kujisimamia.

**JINSI NINAVYOJITAMBUA NA JINSI NINAVYOISHI.**

Hili ni swali lililojadiliwa na kila familia (mume na mke) kwa dakika 45. Baada ya kipindi hicho cha majadiliano, tulipata chakula na mapumziko.

Wakati huu Mch. Ndongo aligawa fomu  kwa wachungaji wamishonari ili wajaze taarifa zao na za familia zao, eneo wanalofanyia kazi, wanapataje mahitaji yao, aina ya usafiri wanaotumia n.k kwa ajili ya kusaidia Ofisi ya Dayosisi, taarifa hizi zitaambatanishwa na picha zao.

**KIPINDI CHA JIONI**

Baada ya kurudi darasani Mch. Ndaro alipewa nafasi ya kueleza juu ya AICT MAPANA Chuo cha Umisionari. Mchungaji Ndaro, wakishirikiana na mkewe, walisoma historia fupi juu ya maono ya MAPANA yalivyoanza na mpaka sasa hatua inayoendelea. MAPANA maana yake ni ***Missions Awareness Programme for African Nations Abondoned.*** Mafundisho haya yanalenga kanisa kupanua wingo na kuzifikia jamii nyingine zilizotelekezwa kwa injili. Hivyo basi mchungaji Ndaro alitoa hamasa kwa wachungaji kuwa, masomo haya yanafaa kwa kila Local-church maana kila mkristo akijifunza masomo haya atakuwa amepata msingi wa Neno sahihi la Mungu, Uongozi, jinsi ya kutayarisha na kuandaa Ibada, Kutembelea na kushauri watu na mafundisho ya dini ya Kiislam na jinsi ya kuwashuhudia habari njema.

Baada ya mafafanuzi hayo, mchungaji Ndaro alimkaribisha mchungaji Masanja ambaye ni mmoja wa wakufunzi wa MAPANA katika darasa la AICT Kinyerezi. Mch. Masanja pia alieleza jinsi ambavyo Masomo haya ni ya muhimu kwa Kanisa hasa kwa kipindi hiki tulichomo sasa. Hivyo alisisitiza kuwa ingekuwa vyema MAPANA ikifundishwa kwa kila Local church. Aliongeza kuwa baada ya masomo ya kitheolojia ya mwaka wa kwanza kwa kutumia kitabu cha Grudem kwa jina ‘Systematic Theology’  tutapata nakala ya Kiswahili ya kitabu hiki, na hayo yatakuwa ni mafaniko muhimu sana kwa chuo na kanisa.

Mwisho Mch. Ndaro alimkaribisha Askofu Salalah ikiwa alikuwa na cha kusema kuhusu masomo hayo. Askofu alisema kwamba,  yeye aliona umuhimu huo ndiyo maana aliruhusu mpango huu katika Dayosisi yake, na alifungua darasa/kituo cha kwanza huko AICT Kizota mwaka 2012 na mwaka huu 2014 amefungua kituo kingine huko AICT KInyerezi. Hivyo basi aliendelea kubariki mpango huu na kusema kuwa **MAPANA** ***kiwe moja ya vyombo vyetuvya injili  katika makanisa yetu kama Dayosisi.***

1. MWENYEKITI WA TAASISI ALIMKARIBISHA MGENI RASMI (MWJ. MARIAM SALALAH)
2. Askofu Salalah alifungua kipind hiki kwa maombi.
3. Mama askofu alipewa nafasi ya kusema neno kabla ya kutoa vyeti.

Alisema kuwa kwa kipindi hiki cha juma hili moja tumefundishwa masomo ya kutusaidia katika safari yetu ya kimwili na kitumishi pia, hivyo basi cheti hiki ni kumbukumbu ya mafundisho ya thamani tuliyoyapokea. Mungu atusaidie kuyaweka maishani na kuyatumia kwa utukufu wa Bwana.

**Mratibu:-** Tony alisoma majina ya wanasemina na mgeni rasmi aliwapa vyeti wahitimu.

Baada ya kutoa vyeti mgeni rasmi mama Ask. Salalah alitoa shukrani kwa kupewa fursa hiyo kisha alifunga kwa maombi na neema ya Bwana.

MRATIBU:-

Aliwashukuru wanasemina kwa kufika na kushiriki semina hii na kuwatia moyo kuwashukuru wapishi kwa kazi yao nzuri ya upishi na huduma kwa ujumla.Aidha aliomba radhi kwa kutumia ukumbi usio rasmi na wenye nafasi ndogo lakini aliwatia moyo kwamba mwakini Mungu akitujalia tutakuwa kwenye ukumbi mpya.

Baada ya michezo.

Tuliimba nyimbo za kusifu kisha mwenyekiti alimkaribisha mchungaiji Ndaro kutoa shukrani kwa wapishi kwa niaba ya wanasemina. Baada ya shukrani hizo tulitaja mambo ya kuombea na kisha kuomba wote kwa pamoja na ndipo Mch. Mabele aliomba kwa ajili ya chakula cha usiku.

**Maombezi.**
Wagonjwa:- Mzee Mabina.
Shukrani- kwa kumaliza semina salama. Taasisi ya Biblia na Utumishi.
Mratibu, mwenyekiti na kamati yote.

**KIPINDI CHA MICHEZO 19/11/2014**

Wachezaji:- Football
1. Kanda ya kati—(waliwafunga Pwani magoli 3)
2. Kanda ya Pwani (Waliwafunga Kanda ya Kati goli 1)

Kocha wa Pwani alikuwa Mch. William Mfeti na kanda ya Kati Mch. Alfred Ndaro

**Tar.20/11/2014**

Timu hizi mbili ziliendelea na siku hiyo kanda ya Pwani walifunga goli moja na kanda ya Kati hawakufunga.

**21/11/2014**

Siku hiyo walicheza vollyball kwani namba ya wachezaji football ilipungua baada ya wengine kuondoka. Katika mchezo huu Pwani waliibuka washindi kwa magoli 3 kwa 1 dhidi ya kanda ya Kati

**Ushindi**
- Kanda ya Pwani --- Washindi wa Vol-lball
- Kanda ya Kati ---- Washindi wa football

Wanawake walishangilia tu. Wao hawakucheza maana walikosa uwanja wa netball. Wengi wao ni wazoefu wa mchezo huo.